LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# HAKI YA RUFAA

## TARATIBU NA MUDA WA RUFAA KATIKA MASHAURI MAHAKAMANI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

**SMS 0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# HAKI YA RUFAA

## TARATIBU NA MUDA WA RUFAA KATIKA MASHAURI MAHAKAMANI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


**1. MAANA YA RUFAA KATIKA MASHAURI YA DAAWA................. 9**

1.1.Rufaa ni Nini?.......................................................................................................... 9

1.2.Haki ya Rufaa inatolewa na Sheria ipi?...................................................................... 9

**2. UTARATIBU WA KUKATA RUFAA KUTOKA BARAZA LA KATA KWENDA BARAZA LA NYUMBA NA ARDHI LA WILAYA.......... 11**

**3. RUFAA KUTOKA MAHAKAMA YA MWANZO KWENDA MAHAKAMA YA WILAYA/HAKIMU MKAZI .................................... 12**

3.1.Utaratibu wa kukata Rufaa toka Mahakama ya Mwanzo kwenda Mahakama ya Wilaya / Hakimu Mkazi............................................................ 12

3.2.Kupeleka Rufaa Nje ya Muda..........................................................................13

**4. RUFAA KUTOKA MAHAKAMA YA WILAYA/HAKIMU MKAZI KWENDA MAHAKAMA KUU ........................................................... 15**

4.1.Hukumu ambayo Huwezi Kukata Rufaa dhidi yake ......................................... 15

4.2.Utaratibu wa kupeleka rufaa Mahakama Kuu ................................................... 15

**5. MUDA WA KUPELEKA RUFAA MAHAKAMA KUU ...................... 16**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususani, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Bi. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama raia angekuwa na uelewa kidogo wa sheria. ni kwa sababu hiyo basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo

ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako upata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam ikiwa na ofisi ndogo Arusha.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# 1. MAANA YA RUFAA KATIKA MASHAURI YA DAAWA

## 1.1. Rufaa ni Nini?

Rufaa ni hatua inayompa mtu au watu walioshindwa kesi/shauri kupinga uamuzi huo katika mahakama yenye mamlaka ya juu zaidi ya ile iliyotoa hukumu ya kushindwa. Katika kesi za madai au jinai, yoyote ambaye hakuridhika na hukumu, anaweza kupinga hukumu yote au sehemu ya hukumu au akapinga kiwango cha fidia/faini kuwa ni kidogo au hakubaliani nacho kabisa.

## 1.2. Haki ya Rufaa inatolewa na Sheria ipi?

Haki ya rufaa inatolewa na sheria mbalimbali hapa Tanzania. Baadhi ya sheria hizo ni kama zifuatazo:

- Kwanza kabisa, haki ya rufaa ni haki inayotolewa na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Hii inapatikana katika Ibara ya 13 ya Katiba yetu;
- Sheria za Mahakama za Mahakimu Na. 2 za mwaka 1984;

- Sheria ya Mwenendo wa Madai ya mwaka 1966;
- Sheria ya Ndoa, ya mwaka 1971;
- Sheria ya Mabaraza ya Ardhi Na.2 ya mwaka 2002.

Kama ilivyoelezwa hapo juu, haki ya kupinga uamuzi uliotolewa na mahakama au na chombo kilichopewa mamlaka ya kutoa haki ni haki ya kikatiba. Hata hivyo, pamoja na kuwa ni haki ya kikatiba, mtu yeyote anayepinga maamuzi lazima afuate taratibu zilizoainishwa na sheria za nchi zinazotoa haki husika. Ni lazima ifahamike kuwa mtu asipozingatia taratibu hizo, basi anaweza kupoteza haki yake ya kukata rufaa.

## 2. UTARATIBU WA KUKATA RUFAA KUTOKA BARAZA LA KATA KWENDA BARAZA LA NYUMBA NA ARDHI LA WILAYA

Mabaraza ya Kata yamepewa uwezo wa kusikiliza masuala ya ardhi kama yalivyo ainishwa na sheria ya Mabaraza ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002.

Hivyo basi, Sheria ya Mabaraza ya Ardhi inasema kuwa, mtu ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa na Baraza la Kata anaweza kukata rufaa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lililopo katika eneo la wilaya iliopo Kata husika.

Katika kupeleka rufaa, muomba rufaa anatakiwa kupeleka sababu za rufaa pamoja na nakala ya uamuzi anaokusudia kuupinga uliotolewa na Baraza la Kata.

Mrufani au mrufaniwa, anaweza kwenda mwenyewe au kuwakilishwa na mtu yeyote asiye mwanasheria atakayemtambulisha kwa kufuata taratibu za sheria.

# 3. RUFAA KUTOKA MAHAKAMA YA MWANZO KWENDA MAHAKAMA YA WILAYA/HAKIMU MKAZI

Mahakama ya Mwanzo imepewa nguvu za kisheria kutatua migogoro mbalimbali isipokuwa masuala ya ardhi kama ilivyo ainishwa na Sheria za Mahakama za Mahakimu ya mwaka 1984 iliyofanyiwa mapitio mwaka, 2002.

Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mahakama ya Mwanzo anaweza kukata rufaa katika Mahakama ya Wilaya/Hakimu Mkazi.

## 3.1. Utaratibu wa kukata Rufaa toka Mahakama ya Mwanzo kwenda Mahakama ya Wilaya / Hakimu Mkazi

Sheria za Mahakama za Mahakimu Na. 2 ya mwaka 1984 iliyofanyiwa mapitio mwaka, 2002 inatoa haki ya kukata rufaa kwa mtu asiyeridhika na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Mwanzo kwenda Mahakama ya Wilaya/Hakimu Mkazi kwa kufuata taratibu zilizowekwa kisheria.

Mrufani anatakiwa kuomba nakala ya hukumu ya Mahakama ya Mwanzo.

Endapo mrufani anachelewa kupata nakala ya hukumu, mrufani anayo nafuu ya kisheria za yeye kuweza kuwasilisha maombi ya rufaa yake nje ya muda.

## 3.2. Kupeleka Rufaa Nje ya Muda

Kumbuka kuwa kisheria ukichelewa kupeleka rufaa yako ndani ya siku 30 tangu hukumu inapotolewa ama unapopata nakala halisi ya hukumu au iliposainiwa (kulingana na mazingira), rufaa yako haitakuwa halali mahakamani.

Hata hivyo, Sheria za Mahakama za Mahakimu Na. 2 ya mwaka 1984 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002, kwa kujua kwamba mrufani anaweza kuwa na matatizo mbalimbali ambayo mengine hayazuiliki, imetoa mamlaka kwa Mahakama za Wilaya/Hakimu Mkazi kuongeza muda huo.

Ili uweze kufanikiwa, lazima maombi yako

yaoneshe kuwa kuna sababu za msingi ambazo zilizuia rufaa yako kupelekwa ndani ya muda.

Katika kukata rufaa katika Mahakama ya Wilaya/ Hakimu Mkazi endapo mrufani hajui kuandika au anajua kuandika, Sheria za Mahakama za Mahakimu imetoa mwanya wa kueleza sababu zake kwa mdomo na Hakimu anawajibika kuandika sababu hizo na kuendelea kusikiliza rufaa hiyo.

# 4. RUFAA KUTOKA MAHAKAMA YA WILAYA/HAKIMU MKAZI KWENDA MAHAKAMA KUU

Mahakama za Wilaya na zile za Hakimu Mkazi, zinanguvu sawa za kisheria. Hivyo taratibu zinazotumika katika mahakama hizi zinafanana. Kwa hiyo, rufaa kutoka Mahakama ya Wilaya/Hakimu Mkazi inaweza kupelekwa Mahakama Kuu.

## 4.1. Hukumu ambayo Huwezi Kukata Rufaa dhidi yake

- Hukumu iliyotokana na makubaliano ya pande zote mbili katika shauri haiwezi kukatiwa rufaa.
- Hukumu iliyotolewa uamuzi kwa kusikilizwa upande mmoja, haikatiwi rufaa.

## 4.2. Utaratibu wa kupeleka rufaa Mahakama Kuu

- Rufaa inapelekwa na hati maalumu yenye sababu za rufaa;
- Hati hiyo inabidi isainiwe na mkata rufaa au/na wakili kama anawakilishwa na wakili;
- Hati ya sababu ya rufaa haitakiwi kuwa na masuala mengi, inatakiwa ieleze sababu kwa ufupi sana kwa lugha inayoeleweka/rahisi;
- Nakala kivuli ya amri inayopingwa na uamuzi.

# 5. MUDA WA KUPELEKA RUFAA MAHAKAMA KUU

Sheria ya Mwenendo wa Madai haijaainisha muda wa kupeleka rufaa katika Mahakama Kuu. Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria ya Muda wa Ukomo wa Madai, rufaa inatakiwa kupelekwa ndani ya siku 45 kuanzia siku hukumu ilipotolewa na mahakama iliyo chini ya Mahakama Kuu pale ambapo suala lilianzia kwenye mahakama hiyo ya chini.

Ikiwa suala linapelekwa Mahakama Kuu kwa rufaa na lilianzia Mahakama ya Mwanzo, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Madai rufaa yake ni siku 30 tu.

Ikumbukwe kuwa kukata rufaa sio sababu ya kusitisha utekelezaji wa hukumu ambayo imeshatolewa. Ili kusitisha utekelezaji wa hukumu iliyotolewa, mrufani anweza kuiomba Mahakama kutoa amri ya kusitisha utekelezaji wa hukumu kama mrufani anatoa sababu za msingi.

Ndugu msomaji, tunatumaini kuwa mpaka sasa umepata ufahamu wa haki na taratibu za kukata rufaa katika Mahakama zetu na vyombo vingine vya kutoa maamuzi nchini. Tunaomba elimu hii uliyoipata uitoe kwa wengine ili waweze kujua ni nini cha kufanya baada ya kupata ya kutoridhika na hukumu/maamuzi ya mahakama na nafuu zinazoweza kupatikana kupitia rufaa.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187;
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*